TANGAZO LA SERIKALI NA. 554 limetangazwa tarehe 17/7/2020

SHERIA YA TAIFA YA UCHAGUZI NA
SHERIA YA UCHAGUZI YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 343 NA 292)

# TANGAZO

*(Limetolewa chini ya kifungu cha 37(1)(a) na 48(1))*

TANGAZO LA SIKU YA UTEUZI WA WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS, UBUNGE NA UDIWANI LA MWAKA 2020

Jina

**1**. Tangazo hili litajulikana kama Tangazo la Siku ya Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais, Ubunge na Udiwani, la mwaka 2020.

Siku ya uteuzi

**2**. Tume ya Taifa ya Uchaguzi inautangazia umma na vyama vyote vya siasa kuwa siku ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais, Ubunge na Udiwani itakuwa tarehe 25 Agosti, 2020 kabla ya saa kumi alasiri.

Utaratibu wa kurejesha fomu

**3**. Watu wote wanaotaka kugombea nafasi ya kiti cha Rais, Ubunge na Udiwani watarejesha fomu za uteuzi kwa Wasimamizi wa Uchaguzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali lililopo kwenye Tangazo hili.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

UREJESHAJI WA FOMU ZA UTEUZI

| Na. | Fomu | Mahala inaporejeshwa |
|---|---|---|
| 1. | Fomu za Uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais | Zirejeshwe Tume ya Taifa ya Uchaguzi |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Fomu za Uteuzi wa Wagombea Ubunge | Zirejeshwe kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo |
| 3. | Fomu za Uteuzi wa wagombea Udiwani | Zirejeshwe kwa Wasimamizi wa Uchaguzi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kwenye makao makuu ya Kata |

Dar es Salaam,
16 Julai, 2020

**SEMISTOCLES S. KAIJAGE**
*Mwenyekiti Tume ya Taifa ya Uchaguzi*